GRADE 5 -YEAR 2022
EXAMINATION: KISWAHILI ACTIVITIES

ZOEZI 1: KUSOMA KWA UFAHAMU
Soma kifungu kifuatacho kisha uyjibu swali la 1 hadi la 7

Mipango yote ya sherehe ya kuzaliwa kwa baba yangu ilikuwa imepangwa ikapangika.Ilikuwa siku ya tatu ya juma. Baba alikuwa akikamilisha miaka thelathini na tisa. Yeye hakuwa amekula chumvi nyingi kama alivyokuwa babaye Meishisana.

Mapochopocho ya vyakula mbalimbali yalikuwa yakinukia mezani na hata mekoni. Vyakula kama vile pilau, biriani , maandazi na vibanzi vilivutia sana machoni pa wageni watano waalikwa. Nilishangaa nilipomwona Bwana Kauleni akidondokwa na mate kwa sababu ya kuitamani keki yenyewe. Watu wengine ambao sikuwatambua kwa majina yao, walikuwa wameketi kitako sebuleni huku wamejipamba kweli kweli. Bila shaka wote walijawa na tabasamu nyusoni pao. Keki yenyewe ilikuwa tamu kama halua. Mimi mwenyewe nilihusika kwa kuwakaribisha marafiki zangu kwenye viti baada ya kuvipanga.

Maswali

1. Je, kisa hiki kinahusu sherehe ya nani?
   _____
2. Sherehe yenyewe ilikuwa siku gani ya juma?
   _____
3. Mwandishi alitumia maneno, "hakuwa amekula chumvi nyingi." Je, hii inamaanisha nini ?
   _____
4. Wageni walikuwa wameketi kitako. Pigia mstari kielezi katika sentensi hii.
   _____
5. Je, sherehe hii ilihudhuriwa na wageni wangapi waalikwa?
   _____
6. Taja jina la babuye mwandishi.
   _____
7. Kifungu ulichokisoma kinahusu nini?
   _____

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 8 hadi la 14.

Mwaka huu ulipoanza, sote tulifurahi kurudi katika shule yetu. Shule hiyo inajulikana kama Mematele. Ina wanafunzi elfu moja na mia mbili na mabasi sita. Mabasi yote ya shule hiyo yamepakwa rangi ya manjano.
Tulipowasili shuleni, tuliingia madarasani na kuketi kwenye viti vyetu. Mwalimu mmoja ambaye tulimpenda sana alingia darasani na kutuamkua, " Hamjambo wanafunzi " Nasi tukajibu, "Hatujambo
mwalimu Matunda. Shikamoo"